چلتی محل کا سودا

Mkataba wa Kasri la Peponi

(Swahili)

Shaikh-e-Tariqat Ameer-e-AhleSunnat
Mwanzilishi wa Dawat-e-Islami,
Allama Moullana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi

جَنَّتِی مَحَل کا سَودا

Mkataba wa Kasri la Peponi

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Aĥl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-islami ʻAllāmaĥ Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَة katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlise Tarajim (Dawat-e-Islami)
Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina, Mahalla Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina, Karachi, Pakistan
Wasiliana kwa nambari: +92-21-34921389 hadi 91
translation@dawateislami.net

Maktaba-tul-Madina

UK: 80-82 Bordesley Green Road, Birmingham, B9 4TA.
Contact: 07989996380 - 07867860092
E-mail: uk@dawateislami.net

USA: Faizan-e-Madina, P. O. Box 36216, Houston, Tx 77274.
Contact: +713-459-1581, 832-618-5101

INDIA: 19/20 Muhammad Ali Road, opposite Mandvi post office
Mumbai – 400 003.
Contact: +91-022-23454429

BANGLADESH: K.M Bhovan, 1st Floor, 11, Andar Killa Chittagong.

HONG KONG: Faizan-e-Madina, M/F-75, Ho Pui Street, Tsuen Wan N.T.
Contact: +85-98750884 – 31451557

SOUTH AFRICA: 61A, Mint Road, Fordsburg, Johannesburg.
Contact: 011-838 9099

KENYA: Kanz-ul-Iman, Near Al-Farooq Hospital, Tonoka Area Mvita,
Mombasa.
Contact: +254-721-521916

TORONTO CANADA: 1060 Britannia Road Unit 20, 21 Mississauga ONT
Canada.
Contact: +141-664-82261

MOZAMBIQUE: Mesquita Faizan-e-Madina Rua Alfredo Lawley, Esturro, Beira.
Contact: 00258-848554888 - 00258-822808580

www.dawateislami.net
Maktaba-tul-Madina of Dawateisla

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ

اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَاالْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

Tafsiri

Ee Mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf juz. I, uk. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara moja kabla na baada ya dua.

Yaliomo

Maktaba-tul-Madina.....ii
Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu..... iii

Mkataba wa Kasri la Peponi.....1

Ubora wa Kumswalia Mtume ﷺ.....1
Sifa Kuu Ya Mawalii.....5
Heshimu Kila Mtu Mwema.....5
Kuangamia Kwa Fidhuli.....6
Ulimwengu Hauna Maana Yeyote Mbele Ya Mawalii.....7
1. Riziki Kwa Ndege.....7
Kutawakali Ni Nini?.....8
2. Ni Bora Kuliko Dunia Na Vilivyomo Ndani Yake.....8
3. Wanaotundiza Mali Kwa Maisha Ya Dunia Hawana Busara.....9
4. Ishi Duniani Kama Msafiri.....10
5. Maadui Hawatakuwa Waoga tena.....10
6. Mapenzi Ya Ulimweng -Kiini cha Dhambi.....12
7. Thamani Ya Ulimwengu Ukiulinganisha Na Ahera 12
8. Mzoga Wa Kondoo.....13

9. Ulimwengu Hauna Hata Thamani Ya Ubawa Wa Mbu....14
10. Kuwa Mbali Na Ibada....14
11. Kuupenda Ulimwengu Husababisha Hasara Ya Ahera....15
12. Chakula Cha Siku Moja....15
13. Dunia Imelaaniwa....15
14. Allah عَزَّوَجَلَّ Humfanya Mwanadamu Kuiepuka Dunia....16
15. Amelaaniwa Mtumwa Wa Mali....16
16. Uharibifu Uletwao Na Kupenda Mali Na Sifa....16
17. Dunia ni Jela Kwa Muislamu....16
Ni Sunna Kufanya Juhudi Za Kibinafsi....17
Umuhimu Wa Juhudi Za Kibinafsi....17
Malipo Ya Ulinganizi Kwa Ajili Ya Njia Ya Haki....18
Malipo Yaliyosawa Na Ibada Ya Mwaka Mzima....19
Visa Viwili Vya Ajabu Kuhusu Juhudi Za Kibinafsi....20
Mbinu Za Kumbadilisha Adui Kuwa Rafiki....22
Kumfanyia Dereva Juhudi Za Kibinafsi....23
Makatazo Mawili Kutoka Kwa Mtume Mtukufu ﷺ....24

1. Amekataza Kujenga Nyumba Bila Dharura.....24
2. Hakuna Kheri Kujenga Bila Dharura 25
Onyo Kutoka Kwa Bwana Wa Mawalii.....26
Walii wa Mwenyezimungu Alipomuona Mtu Akijenga Nyumba.....26
Kisa Chenye Mazingatio 26
Chumo La Miaka 100 Lisilo Na Uhakika Mbeleni.....27
Ni Mahali Pa Mazingatio 27
Yako Wapi Majumba Yakupendeza?.....28
Tafakari Juu Ya Maisha Ya Ahera 29
Ni Bora Kuliko Miaka Sitini Ya Ibada 30
Maiti Ya Siku 70.....30
Marejeleo 32

www.dawateislami.net
I.T. Majlis of Dawateislami

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

Mkataba wa
Kasri la Peponi

Ijapokuwa shetani atataka kukuzuia kusoma kitabu hiki, kisome chote. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ utapata fikra ya ahera.

Ubora Wa Kumswalia Mtume ﷺ

Mtume wa Raḥmaĥ, mtetezi wa Ummaĥ, mmiliki wa pepo صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, “Wanaopendana kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ wanapokutana na kupeana mikono huku wakimswalia Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, husamehewa madhambi yao yaliyopita na yatakayokuja kabla hawajaachana. *(Musnad Abī Ya’lā, uk. 95, juz. 3, Ḥadīš 2951)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Mjini Basra, Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَفَّار alipitia kasri lililokuwa likijengwa na akaingia ndani. Alimuona kijana mzuri akiwaongoza wafanyikazi na vibarua kuhusu ujenzi. Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَفَّار akamuita mwenzake

Sayyidunā Ja'far Bin Sulaymān عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْحَنَّان na akamuambia, "Tazama namna kijana yule anavyojishugulisha na ujenzi wa kasri. Ninamuonea huruma na ninataka kumuomba Allah عَزَّوَجَلَّ amuweke huru kutokana na hali ile, pengine huenda akawa mmoja kati ya vijana wa peponi. Halafu akamfuata pamoja na Sayyidunā Ja'far Bin Sulaymān عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْحَنَّان na akamsalimia. Awali kijana yule hakumtambua Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار. Walipojitambulisha, kijana aliwapa heshima kubwa na kwa upole na adabu akawauliza lengo lao la kufika pale.

Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akmuuliza, "Umeamua kutumia kiasi gani katika kujenga na kulipamba kasri hili?" Akajibu, "Dirham laki moja." Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akasema, "Ukinipa dirham laki moja, nakuahidi kasri zuri zaidi na lenye kudumu. Mchanga wa kasri hilo utakuwa ni wa miski na zafarani na itabaki milele halitavunjika. Zaidi ya kasri hilo, pia kutakuwa na wafanyikazi, kuba lililotengenezwa kwa rubi na mahema mazuri. Kasri hilo halikujengwa na mjenzi yeyote bali kwa amri ya Allah عَزَّوَجَلَّ-Kun (kuwa)!"

Kijana akamuomba Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار kumpa usiku mmoja kulifiliria jambo hilo. Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akakubali. Baada ya mazungumzo akaregea. Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار alimfikiria kijana yule usiku mzima na akaendelea kumuombea.

Asubuhi yake, Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار alipofikia kasri lile, alimkuta kijana anamngojea. Kwa moyo mkunjufu,

alimkaribisha Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار na akamwambia kwa upole na adabu, “Je, unakumbuka ulichoniahidi kunipa jana?” Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akajibu, “Ndiyo.” Kijana akampa Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار dirham laki moja ambayo ilikuwa ni akiba yake yote. Halafu akampa Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار kalamu, kichupa cha wino na karatasi.

Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akaandika mkataba kwa maneno yafuatayo: “بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم Mālik Bin Dīnār anasimamia udhamini wa kupewa kasri na Allah عَزَّوَجَلَّ fulani wa fulani kwa kubadilishana naye nyumba yake ya duniani. Iwapo kutakuwa na mapambo zaidi, itakuwa ni rehema ya Allah عَزَّوَجَلَّ.

Baada ya kumkabidhi kijana yule ule mkataba, Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار akachukua dirham laki moja kutoka kwake na kufikia jioni alikuwa ameshazigawanya kwa mafukara na maskini.

Baada ya karibu siku 40, Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار alipokuwa akitoka msikitini baada ya kuswali swala ya alfajiri, aliona kijikaratasi kiblani. Ilikuwa ni mkataba ule ule alioandikiana na kijana yule. Maneno yafuatayo yaliandikwa nyuma ya karatasi bila kutumia wino: “Hii ni barua ya uhuru kwa Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ. Tumemjaalia kijana kasri

ambalo ulimuhakikishia kwa (kutumia) jina letu na tumeliongeza mara 70.”

Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار aliichukua karatasi na kwa haraka aliifikia nyumba ya kijana (yule). (Huko) alisikia vilio. Alipouliza, aliambiwa kuwa kijana alikufa siku iliyotangulia. Muosha maiti alisema, “Alipokuwa akiweka wasia wake, aliniomba nimuoshe halafu akanipa kijikaratasi nikiweke katika sanda yake.” Kwa hivyo alizikwa kulingana na wasia wake. Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار alipomuonyesha karatasi aliyoipata katika kibla cha msikiti, muosha maiti akasema, “Kwa uweza wa Allah عَزَّوَجَلَّ, ni karatasi ile ile niliyoiweka kwa mikono yangu mwenyewe katika sanda.” Mtu mmoja alipokuja kukijua kisa (hicho) chote alijitolea kumpa Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار dirham laki mbili ili apewe mkataba wa kasri la peponi. Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار akakataa na akasema, “Lililoandikwa limetokea, Allah عَزَّوَجَلَّ, hutenda analotaka.” Halafu Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار alilia sana akitafakari kuhusu kijana aliyekufa. *(Rauḍ-ur-Riyāḥīn, uk. 58-59)*

Allah عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe bila hesabu kwa baraka zao!

آمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Sifa Kuu Ya Mawalii

Ndugu wapenzi waislamu! Je, munaona namna gani Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ alivyompa mamlaka Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَقَّار ya kuweka mkataba wa kasri la peponi kwa nyumba ya duniani. Bila shaka shani ya mawalii wa Allah عَزَّوَجَلَّ ni kubwa mno. Soma hadithi ifuatayo ili uone sifa kuu ya mawalii wa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Riyaa kidogo (kufanya amali njema kwa ajili ya kupata sifa kwa watu) ni shirki, na mwenye kufanya uadui na walii wa Allah عَزَّوَجَلَّ hupigana vita dhidi ya Allah عَزَّوَجَلَّ. Allah عَزَّوَجَلَّ anawapenda watu wema, wacha Mungu wanaojificha. Ambao wakipotea, hakuna anayewatafuta; wakiwepo hakuna anayewathamini; nyoyo zao ni taa za uongofu na wamejitenga na fitna yenye giza na vumbi. *(Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, uk. 269, juzuu. 2, Ḥadīš, 5328)*

Heshimu Kila Mtu Mwema

Ndugu wapenzi waislamu! Ni wazi kwamba umaarufu wa duniani na kusifiwa na watu si kigezo cha kuwa rafiki wa Allah عَزَّوَجَلَّ. Bali wale ambao wana ikhlasi (wenye kutaka radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ) tu ndiwo ambao ni marafiki wa Allah عَزَّوَجَلَّ hata ikiwa duniani watu hawawathamini. Wakipotea hakuna anayewatafuta; wakifariki hakuna anyehuzunika; na wanapohudhuria hafla, hakuna anayewauliza. Hata hivyo inatakiwa tumuheshimu kila muislamu, la sivyo, basi angalao

tusimdharau kwani huenda akawa ni walii wa Allah عَزَّوَجَلَّ aliyefichika. Na tukimdharau, huenda tukadhurika.

Kuangamia Kwa Fidhuli

Mvua ilikuwa imepungua, upepo mwanana ulikuwa ukivuma. Mcha Mungu aliyekuwa, amevaa matambara na viatu vibovu alipita sokoni(huku akimsabihi Allah عَزَّوَجَلَّ). Alipopitia duka liuzwalo vitamutamu, muuzaji vitamutamu alimpa kikombe cha maziwa. Alikaa, akasema بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم na akanywa. Alipomaliza akamshukuru عَزَّوَجَلَّ, na akaendelea na safari.

Mcha Mungu akapita barabarani karibu na nyumba ya malaya ambaye alikuwa amekaa nje na mpenziwe. Kwa ajili ya mvua kunyesha, barabarani kulikuwa na matope. Mcha Mungu, bila kukusudia alikanyaga matope yakamrukia na kumchafulia malaya nguo yake. Mpenzi wake akakasirika na akampiga kofi Mcha Mungu. Mcha Mungu akamshukuru Allah عَزَّوَجَلَّ na akasema: “Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Hakika mambo yako ni ya ajabu! Kuna wakati hupata maziwa na wakati mwengine hupigwa makofi. Hata hivyo nimeridhia radhi zako.” Baada ya kusema hayo, akaendelea na safari yake.

Baada ya muda, mpenzi wa yule malaya alipanda juu ya paa na akateleza na akaanguka chini kichwa kichwa na akafa. Mara ya pili Mcha Mungu alipopita pale, mtu mmoja akamwambia, “Ulimuapiza ndio maana amekufa.” Mcha Mungu akamjibu, “Naapa kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ sikumuapiza. Alinipiga kofi kwa

ajili ya mpenzi wake (malaya) basi Allah عَزَّوَجَلَّ naye akalipiza kisasi kwa ajili ya mpenzi wake (mcha Mungu).

Ulimwengu Hauna Maana Yeyote Mbele Ya Mawalii

Ndugu wapenzi waislamu! Kisa cha 'Mkataba Wa Kasri La Peponi' kinaonyesha utukufu wa mawalii na kwamba wao hawana hamu na ulimwengu bali hamu yao kubwa ni kuubadilisha umma. Hushikwa na wasiwasi kwa ajili ya watu kupuuza dini na kughurika na ulimwengu. Bila shaka ulimwengu hauna maana yoyote mbele yao; hadithi zinazoeleza kuhusu madhara ya dunia zilikuwa mbele ya macho yao. Hebu sikilizeni hadithi kumi na saba zinazoshutumu dunia.

1. Riziki Kwa Ndege

Amīr-ul-Muminīn Sayyidunā 'Umar Fārūq A'ẓam رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنْہُ alimsikia Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akisema, "Ukimtegemea Allah عَزَّوَجَلَّ haki ya kumtegemea, basi atakupa riziki kama anavyowapa ndege ambao hutoka na njaa asubuhi na wakiregea jioni huwa wameshiba." *(Sunan-ut-Tirmizī, uk. 154, juzu 4, Ḥadīš 2351)*

Mfafanuzi maarufu wa Qur'an Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْحَنَّان amesema, "Haki ya kumtegemea Allah عَزَّوَجَلَّ ni kumuamini kuwa yeye pekee ndiye mtoaji wa riziki." Wanavyuoni wengine wamesema, "Haki ya kumtegemea Allah عَزَّوَجَلَّ ni kufanya bidii (kutafuta riziki), kupata au kukosa ni kupenda kwake Allah عَزَّوَجَلَّ. Mtu afanye bidii (kutafuta riziki)

lakini awe na imani juu ya Allah عَزَّوَجَلَّ. Imethibitishwa kwamba wale wanaomtegemea Allah عَزَّوَجَلَّ hawafi njaa.”

Tuzingatie kuwa ndege katika kutafuta riziki hutoka viotani mwao. Hata hivyo miti haiwezi kutembea, lakini hupata maji, mbolea na mahitaji yao mengine. Yai la kurabu linapoangua kinda, kinda kawaida huwa rangi nyeupe hivyo basi wazazi wake humkimbia kwa sababu ya kumuogopa. Kwa amri ya Allah عَزَّوَجَلَّ, aina fulani ya vidudu hujikusanya mdomoni mwa kinda, naye huwala. Manyoya yake yanapogeuka kuwa meusi wazazi wake huregea. *(Mirāt-ul-Manājīḥ, uk. 113-114, juz. 7; Mirqāt, uk. 156, juz. 9, Ḥadīš, 5299)*

Kutawakali Ni Nini?

A’lā Ḥaḍrat Maulānā Shāĥ Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمٰن amesema, “Kutawakali si kuacha njia za kutafutia riziki bali ni kutotegemea njia hizi. *(Fatāwā Razawiyyaĥ, uk. 379, juzuu. 24)* Yaani, mtu azitumie njia hizi (kutafuta riziki) lakini asizitegemee (bali amtegemee Allah عَزَّوَجَلَّ).

2. Ni Bora Kuliko Dunia Na Vilivyomo Ndani Yake

Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, “Eneo (dogo) kima cha mjeledi peponi ni bora kuliko ulimwengu wote na vilivyomo ndani yake. *(Ṣaḥīḥ Bukhārī, uk. 392, juz. 2, Ḥadīš 3250)*

ʻAllāmaĥ Shaykh ʻAbdul Ḥaq Muḥaddiš Diĥlvī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِى akitoa maoni kuhusu hadithi hii amesema, “Sehemu ndogo peponi ni bora kuliko dunia na vitu vyake. Kutaja mjeledi ni kurejelea desturi za kale ambapo mpanda farasi akiamua kushuka mahali, hurusha mjeledi wake ili iwe alama ya mashukio yake na mtu mwengine asishuke pale.” *(Ashi’a-tul-Lam’āt, uk. 433, juz. 4)*

Mfafanuzi maarufu wa Qur’an Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْحَنَّان amesema, kutaja mjeledi ina maana ya eneo dogo la ahera. Kweli malipo ya ahera ni ya kudumu ilihali vitu vya duniani havidumu. Raha za dunia huja na matatizo, ilihali raha za ahera ni safi (hazikuchanganyika na matatizo). Vitu vya duniani ni duni ilihali vya ahera ni bora. Kwa hivyo ulimwengu hauwezi kufananishwa kamwe na mahali padogo peponi. *(Mirāt-ul-Manājīḥ, uk. 447, juz. 7)*

3. Wanaotundiza Mali Kwa Maisha Ya Dunia Hawana Busara

Sayyidatunā ʻĀishaĥ Ṣiddīqaĥ رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْهَا, mama wa waumini amesema kuwa alimsikia Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akisema, “Ulimwengu ni nyumba kwa wale ambao hawana nyumba na ni utajiri kwa wale ambao hawana utajiri na anayetundiza kwa ajili yake hana busara.” *(Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, uk. 250, juz. 2, Ḥadīš 5211)*

4. Ishi Duniani Kama Msafiri

Sayyidunā ʻAbdullāĥ Bin ʻUmar رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُمَا amesimulia, “Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم siku moja alinishika mkono na akasema, “Ishi duniani (ukiwa) kama mgeni na msafiri.” Sayyidunā Ibn ʻUmar رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُمَا amesema, “Ukiwa hai asubuhi, basi usingojee jioni na ukiwa hai jioni basi usingojee asubuhi na ujitayarishe kwa ugonjwa na kifo katika uzima na uhai wako.” *(Ṣaĥīĥ Bukhārī, uk. 223, juz. 4, Ḥadīš 6416)*

5. Maadui Hawatakuwa Waoga tena

Sayyidunā Šaubān رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ amesimulia kwamba Mtume kipenzi na aliyebarikiwa صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Yawezekana mataifa mengine yataalikana (kuwavamia) kama vile mtu anayekula (anavyowaalika) wengine kwa sinia yake (kuja kula) Mtu mmoja akauliza kwa unyenyekevu, “Je, tutakuwa wachache kwa hesabu?” Mtume Mtukufu, صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akajibu kwamba mutakuwa wengi mno lakini mutasombwa kwenye mafuriko kama takataka. Ushujaa, ushupavu na nguvu zenu zitafikia kikomo na Allah عَزَّوَجَلَّ ataondosha hofu katika nyoyo za maadui zenu na katika nyoyo zenu ataitia ‘Waĥn’ (udhaifu). Mtu mmoja akauliza, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم! “Waĥn ni nini?” Mtume wa Mwenyezi Mungu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akasema, “Ni kuupenda ulimwengu na kuogopa kufa.” *(Sunan Abī Dāwūd, uk. 150, juz. 4, Ḥadīš 4297)*

Akishereheshea hadithi hiyo, mfafanuzi maarufu wa Qur’an Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَیْہِ رَحْمَۃُ اللّٰہِ الْحَنَّان amesema, “Nguvu

mbalimbali za makafiri, makiristo, mayahudi na maparisi zitaungana ili kuwaangamiza na hata wataalikana kuwagandamiza, kuwaua, na kuwateketeza waislamu. Hali hii imeshatokea! Tazama mayahudi na makiristo ni maadui lakini wameungana kuwaangamiza waislamu duniani na makafiri wengine pia wanawaunga mkono. Kila neno alilozungumza Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni la kweli. Je, makafiri watakuwa jasiri na shupavu kwa sababu tutakuwa wachache katika kipindi hicho? La! Mutakuwa wengi lakini mutakuwa kama takataka katika bahari kwa sababu ya majivuno, uwoga, utengano, wasiwasi, uvivu, ukosefu wa busara, hofu ya kifo na mapenzi ya ulimwengu. *(Mirqāt, uk. 232, juz. 9, Ḥadīš 5369)*

Hofu juu yenu itaondolewa katika nyoyo za makafiri kwa sababu ya udhaifu. 'Waĥn' inamaana ya uzembe au udhaifu. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sura tul-Luqmān aya ya 14:

حَمَلَتْهُ اُمُّهٗ وَهْنًا عَلٰى وَهْنٍ

Mama yake ameichukua
mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu.

(Juzuu ya 21, Sura-tul-Luqmān, aya ya 14)

Vile vile, Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sura tul-Maryam juzuu ya 16:

رَبِّ اِنِّیۡ وَهَنَ الۡعَظۡمُ مِنِّیۡ

Mola wangu, bila shaka mifupa yangu imekuwa dhaifu.

(Juzuu ya16, Sura-tul-Maryam, aya ya 4)

Ina maana kuwa mutakuwa dhaifu na wazembe na mutaikimbia Jihad. Kuna sababu mbili za udhaifu na uzembe (1) Kuupenda mno ulimwengu na (2) Kuogopa kifo. Taifa lenye kasoro hizi haliwezi kuheshimika. *(Mirat, uk. 173-174, juzuu ya 7)*

6. Mapenzi Ya Ulimweng -Kiini cha Dhambi

Sayyidunā Ḥużayfaĥ رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنۡہُ ameeleza kwamba alimsikia Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akisema katika hotuba yake, “Pombe ndiyo makusanyo ya madhambi” (inafanya watu kufanya dhambi nyingine), wanawake ni kamba za shetani na mapenzi ya dunia ni kichwa cha madhambi yote.” *(Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, uk. 250, juz. 2, Ḥadīš 5212)*

7. Thamani Ya Ulimwengu Ukiulinganisha Na Ahera

Sayyiduna Mustaurid Bin Shaddad رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنۡہُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Naapa kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ! Ukilinganisha na ahera, maisha ya ulimwengu huu ni mafupi mno mfano wa mtu anayetia kidole chake baharini halafu akitazame ni kiasi gani cha maji kilichobaki katika kidole.” *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1529, Ḥadīš 2858)*

Akieleza hadithi hiyo, mfafanuzi wa Qur'an Mufti Aḥmad Yar Khan عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْحَنَّان amesema, "Mlinganisho huu katika hadithi ni kuwafanya watu waelewe zaidi lakini kwa hakika huwezi kufananisha chenye kubaki milele (ahera) na chenye kumalizika (dunia) kwa mfano wa kidole kilicholowa maji na bahari.

Kumbuka! Dunia ni ile ambayo humsaulisha mtu Mola wake. Mtu mwenye busara na mwenye kumjua Allah عَزَّوَجَلَّ dunia yake ni shamba la ahera ilihali hata swala inayoswaliwa na mtu aliyeghafilika kwa ajili ya kuonyesha watu huhesabiwa kuwa sehemu yake ya dunia. Kwa upande mwengine kwa mtu mwenye busara; kula, kunywa, kulala, kuamka, kutembea, kuishi, na hata kufa kwake huhesabiwa kuwa sehemu ya dini kwani matendo haya ni sunna za Kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Muislamu afaa kula, kunywa, kulala na kuamka kwa nia ya kufuata sunna. Kuna tofauti kubwa kati ya maisha ya dunia, maisha duniani na maisha kwa ajili ya dunia. Maisha ya duniani kwa ajili ya ahera wala si kwa ajili ya dunia yamebarikiwa.

8. Mzoga Wa Kondoo

Sayyidunā Jābir رَضِیَ اللّٰهُ تَعَالٰی عَنْهُ ameeleza kuwa Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم aliupita mzoga wa kondoo halafu akasema, "Je, kuna yeyote ambaye angependa kuuchukua mzoga huu kwa dirham moja?" Wakajibu kwa unyenyekevu, "Hatutachukua hata tukipewa bure" Halafu Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, "Naapa kwa Allah عَزَّوَجَلَّ! Dunia ni duni zaidi kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kuliko mzoga huu ulivyo kwenu." *(Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, uk. 242, juz. 2, Ḥadīš 5157)*

Akisherehesha hadithi hii Muftī Ahmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْحَنَّان amesema, “Hakuna anayenunua mzoga wa kondoo hata kwa senti 25 kwa kuwa ngozi yake haina maana na nyama yake ni haramu. Mtu azingatie maana ya dunia kama inavyoelezwa katika hadithi. Masufi wanasema kuwa mawalii wote wa ulimwenguni hawawezi kumbadilisha mtu anayeupenda ulimwengu ilihali mashetani wote hawawezi kumpoteza muislamu muongofu. Mwenye kuipenda dunia, hata akifanya mambo ya dini hufanya kwa ajili ya dunia ilihali mwenye kupenda dini hujihusisha na matendo ya dunia kwa ajili ya dini.” *(Mirāĥ, uk. 3, juz. 7)*

9. Ulimwengu Hauna Hata Thamani Ya Ubawa Wa Mbu

Sayyidunā Saĥl Bin Sa’d رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kuwa, Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Lau dunia ingekuwa na thamani ya ubawa wa mbu kwa Allah عَزَّوَجَلَّ, hangempa kafiri hata tama la maji kunywa.” *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 143, juz. 4, Ḥadīš 2327)*

10. Kuwa Mbali Na Ibada

Sayyidunā Ma’qil Bin Yasār رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ amesema Mtume Kipenzi na aliyebarikiwa صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Muumba wako amesema, “Ewe mwana wa Adamu! Kuwa huru kuniabudu mimi, nitaujaza moyo na kukinai na nitaijaza mikono yako na riziki. Na Ewe mwana wa Adamu! Ukiacha kuniabudu mimi nitaujaza moyo wako ufukara na nitaishughulisha mikono yako na kazi za kidunia.” *(Al-Mustadrak, uk. 464, juz. 5, Ḥadīš 7996)*

11. Kuupenda Ulimwengu Husababisha Hasara Ya Ahera

Sayyidunā Abū Mūsā Ash'arī رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume wetu kipenzi aliyebarikiwa صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Anayeupenda ulimwengu husababisha madhara kwa ahera yake na anayependa ahera huudhuru ulimwengu wake. Kwa hivyo yatangulize maisha ya ahera ambayo ni ya milele juu ya dunia ambayo si ya milele." *(Al-Mustadrak, uk. 454, juz. 5, Ḥadīš 7967)*

12. Chakula Cha Siku Moja

Sayyidunā 'Ubaīdullāĥ Bin Miḥṣan Khaṭmī رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ alitoa habari kuwa Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Yule ambaye kati yenu ameamka asubuhi na afya, moyo wake umetulia na ana chakula cha siku moja; basi ni kama ambaye amekusanyiwa ulimwengu mzima." *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 154, juz. 4, Ḥadīš 2353)*

صَلُّوْا عَلَی الْحَبِیْب صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلٰی مُحَمَّد

13. Dunia Imelaaniwa

Sayyidunā Abū Ĥuraīraĥ رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Tahadhari! Dunia na vilivyomo ndani yake vimelaaniwa isipokuwa kumkumbuka Allah عَزَّوَجَلَّ na kila ambacho kinamfanya mja kuwa karibu na Allah عَزَّوَجَلَّ na mwenye elimu na mwenye kujifunza elimu." *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 144, juz. 4, Ḥadīš 2329)*

14. Allah عَزَّوَجَلَّ Humfanya Mwanadamu Kuiepuka Dunia

Sayyidunā Maḥmūd Bin Lubaīd رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume wa Rehema, Muombeaji umma msamaha, صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Allah عَزَّوَجَلَّ humfanya mja wake kuiepuka dunia kama vile unavyomuepusha mgonjwa wako kula vyakula na vinywaji vinavyodhuru.” *(Shu’ab-ul-Īmān, uk. 321, juz. 7, Ḥadīš 10450)*

15. Amelaaniwa Mtumwa Wa Mali

Sayyidunā Abū Ĥuraīraĥ رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kuwa Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Amelaaniwa mtumwa wa dirham na dinar (pesa).” *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 166, juz. 4, Ḥadīš 2382)*

16. Uharibifu Uletwao Na Kupenda Mali Na Sifa

Sayyidunā Ka’b Bin Mālik رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kuwa Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Mbwa mwitu wawili wenye njaa waliofunguliwa katika kundi la mbuzi hawawezi kuleta hasara kubwa kama inavyoleta tamaa ya mali na sifa kwa imani ya mtu.” *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 166, juz. 4, Ḥadīš 2383)*

17. Dunia ni Jela Kwa Muislamu

Sayyidunā Abū Ĥuraīraĥ رَضِیَ اللہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kuwa Mtume Mtukufu صَلَّی اللہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Dunia ni jela kwa muislamu na pepo kwa kafiri.” *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1582, Ḥadīš 2956)*

Ni Sunna Kufanya Juhudi Za Kibinafsi

Ndugu Wapenzi Waislamu! Kwa kusoma kisa cha kwanza, umeweza kuona namna gani Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْغَفَّار alivyofanya juhudi za kibinafsi kwa njia nzuri. Alimuelekeza kwa fikra ya Kimadani kijana ambaye alikuwa amejishughulisha kujenga jumba la kidunia kwa kuwekeana mkataba wa kasri la peponi. Hakika juhudi za kibinafsi ni muhimu mno katika kufaulu kwa ulinganizi katika njia ya haki. Mitume wote عَلَيْهِمُ السَّلَام akiwemo Mtume Wetu صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم walifanya juhudi za kibinafsi katika kulingania watu katika njia ya Allah.

Umuhimu Wa Juhudi Za Kibinafsi

Ndugu wapenzi waislamu! Karibu asilimia 99 ya kazi za Madani za Dawat-e-Islami zinategemea juhudi za kibinafsi. Juhudi za kibinafsi zimethibitika kuwa na matokeo bora zaidi kuliko juhudi za jumuia. Imeonekana kwamba ndugu waislamu ambao huhudhuria ijtimai ya kila wiki kwa miaka mingi na hutia nia kutokana na kushawishika na bayana; kufanya amali njema kama vile kuswali swala tano kwa jamaa, kufunga mwezi wa Ramadhani, kuvaa kilemba, kufuga ndevu na kuweka nywele kwa mujibu wa sunna, kuvaa nguo na vazi jeupe la Kimadani, kujaza kitabu cha Madani in'amat kila wiki kwa kufanya Fikr-e-Madīnaẖ, kuhudhuria kozi za: Madanī Tarbiyyat kama ile ya siku 63, Madanī Qāfilaẖ ya siku 41, kusafiri na Madanī Qāfilaẖ kwa miezi 12, siku 30, siku 12 au siku 3 na kadhalika. Lakini

wengi hushindwa kutenda kwa mujibu wa nia zao. Kwa upande mwengine ikiwa mlinganizi wa Dawat-e-Islami, kwa kufanya juhudi za kibinafsi kwa upole na busara kwa ndugu muislamu kama huyo na kumshawishi vilivyo, hubadilika na kuanza kufanya kazi za Kimadani. Yaani chuma huyayushwa kwa juhudi za pamoja na hufuliwa kwa umbo la Kimadani kwa juhudi za mtu binafsi.

Kumbuka! Juhudi za kibinafsi ni rahisi zaidi kuliko juhudi za jumuia kwa sababu kila mmoja hana uwezo wa kutoa bayana yenye kufaa mbele ya umati wa watu ila kila mmoja ana uwezo wa juhudi za kibinafsi ingawa huenda akawa si hodari wa kutoa bayana. Pata hazina ya thawabu kwa kuwalingania watu katika haki kwa kupitia juhudi za mtu binafsi.

Malipo Ya Ulinganizi Kwa Ajili Ya Njia Ya Haki

Katika Surah Ḥā-Mim As-Sajdah, juzuu ya 24, aya ya 33 inasema:

وَمَنْ اَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَآ

اِلَى اللّٰهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَّقَالَ اِنَّنِیْ مِنَ الْمُسْلِمِیْنَ ﴿۳۳﴾

Na ni nani asemae kauli bora zaidi kuliko aitae kwa Mwenyezi Mungu, na akafanya vitendo vizuri na husema: "Hakika mimi ni miongoni mwa waislamu."

Kipenzi chetu Mtume mwenye rehema صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Naapa kwa Allah عَزَّوَجَلَّ! Ikiwa Allah عَزَّوَجَلَّ atatoa hidaya

[muongozo] hata kwa mtu mmoja kupitia kwako, (basi) ni bora kwako kuliko ngamia wekundu." *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1311, Ḥadīš 2406)*

Sayyidunā Anas Bin Mālik رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume wa rehema, Muombeaji msamaha umma, Mmiliki wa pepo صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Anayemuongoza mtu kufanya amali njema ni kama (yule ambaye) amefanya amali njema." *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 305, juz. 4, Ḥadīš 2679)*

Sayyidunā Abū Ĥuraīraĥ رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume kipenzi na mweneye rehema صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Anayeita watu katika uongofu atalipwa malipo sawa na wale wanaofuata uongofu huo; na hakutakuwa na upungufu wa malipo kwa wale wanaofuata uongofu huo. Na yule anayeita watu katika upotofu atakuwa na madhambi sawa na wale wanaofuata upotofu huo na hakutakuwa na upungufu wa madhambi ya wale wanaofuata upotofu huo. *(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1438, Ḥadīš 2674)*

Malipo Yaliyosawa Na Ibada Ya Mwaka Mzima

Siku moja Sayyidunā Mūsā Kalīmullāĥ عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام alimuuliza Allah عَزَّوَجَلَّ kwa unyenyekevu, "Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Ana malipo gani anayemuamrisha mema ndugu yake na kumkataza (kutenda) maovu?" Allah عَزَّوَجَلَّ akasema, "Humuandikia malipo ya ibada ya mwaka mmoja kwa kila neno analotamka; na huona haya kumpa adhabu ya Jahanamu." *(Mukāshafa-tul-Qulūb, uk. 48)*

Visa Viwili Vya Ajabu Kuhusu Juhudi Za Kibinafsi

Ndugu wapenzi waislamu! Juhudi za kibinafsi zimechangia pakubwa maendeleo ya Dawat-e-Islami. Sikilizeni visa viwili vya Amir-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه kwa kauli yake mwenyewe kuhusu juhudi za kibinafsi:

1. “Wakati wa mwanzo wa Dawat-e-Islami, nilikuwa nikitembelea watu majumbani, maofisini na madukani ili kufanya juhudi za kibinafsi. Wakati huo nilikuwa imamu katika Masjid Nur, Soko la Makaratasi Karachi. Siku moja kijana (aliyekuwa hana ndevu) aliacha kuswali msikiti niliokuwa mimi ni imamu kwa sababu ya kuudhika kwa kukosa maelewano na mimi. Siku moja nikakutana naye amesimama kando huku akizungumza na rafiki yake. Nikawatolea salamu lakini hakujibu bali aligeuza uso. Halafu nilimuita jina lake na nikamwambia, “Yaonekana umenikasirikia sana.” Nikampiga pambaja. Hasira zake zikapungua na akaeleza yalio moyoni mwake kunihusu. Nilimuondoshea tashwishi yake kwa uzuri. Baadaye akaondoka na rafiki yake.

   Baada ya siku chache, nilimuona rafiki yake na akaniambia kuwa mwenzake alisema, “Ilyās ni mtu wa ajabu; alinitolea salamu lakini nikageuza uso. Badala ya kukasirika alinikumbatia. Nilihisi chuki juu yake moyoni mwangu ikiondolewa na kubakishwa mapenzi. Sasa nitakuwa mfuasi wake tu. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ! Alikuwa mfuasi na mpenzi

mkubwa wa Amīr-e-Aĥl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه na pia alipamba uso wake kwa sunna ya ndevu.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

2. Siku hizo nilikuwa imamu katika msikiti wa Shahīd Kharadar Karachi, na nilikuwa nikitembelea sehemu mbalimbali ili kuwapasha watu habari kuhusu Dawat-e-Islami kupitia bayana zangu. Kwa rehema za Allah عَزَّوَجَلَّ, kazi ya Dawat-e-Islami ilikuwa inaendelea lakini pole pole kama mmea dhaifu.

Nilikuwa nikiishi Musa Lane, Liyari Karachi. Jirani yangu mmoja alinikasirikia kwa sababu ya ukosefu wa kuelewana na akaanza kunitafuta kwa hasira mpaka akafika msikiti wa Shahīd. Wakati huo nilikuwa siko. Nilikuwa nimetoka kwenda kulingania watu. Alinizungumza vibaya mbele ya watu na akatishia kuniaibisha. Nilipojulishwa kuhusu tukio hilo, sikulipiza kisasi wala kuvunjika moyo bali niliendelea na kazi zangu za Madani kama kawaida.

Baada ya siku chache, nilipokuwa nikiregea nyumbani, nilimuona barabarani pamoja na wenzake. Huu ulikuwa ni wakati wangu wa majaribu. Nilijipa moyo na nikatoa salamu lakini aligeuza uso. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ! Sikukasirika bali nilimkumbatia na nikamuita kwa jina lake kwa mapenzi. Halafu nikasema, “Umenikasirikia mno!” Hasira zake zote zikatoweka na kwa ghafla akazungumza, “La ndugu Ilyas,

sina hasira na wewe!" Akanishika mkono na akaniambia, "Twende nyumbani, ni lazima tunywe pamoja kinywaji baridi." اَلْحَمْدُلِلّٰه عَزَّوَجَلَّ! Alinipeleka kwake na kunihudumia.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Mbinu Za Kumbadilisha Adui Kuwa Rafiki

Ndugu waislamu! Kumbuka kanuni hii: uchafu hauwezi kusafishwa kwa uchafu bali husafishwa kwa maji masafi. Kwa hivyo kuwa na adabu hata kama mtu atakukosea adabu. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Utafurahika utakapoona matokeo mazuri. Naapa kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ! Wanabahati wale wanaopambana na uovu kwa uzuri na kuwasamehe wagandamizaji badala ya kulipiza kisasi. Sura Ḥa-Mim As-Sajda juzuu ya 24, aya ya 34 inatuhimiza kuhimili maovu kwa kufanya wema. Inasema:

اِدْفَعْ بِالَّتِیْ هِیَ اَحْسَنُ فَاِذَا الَّذِیْ بَیْنَكَ وَبَیْنَهٗ عَدَاوَةٌ كَاَنَّهٗ وَلِیٌّ حَمِیْمٌ ﴿۳۴﴾

Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa mema); tahamaki Yule ambaye baina yako na yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu. *(Juzuu ya 24, Sūraĥ Ḥā-Mīm, aya 34)*

Nimeelezea visa viwili vinavyonihusu ili kuwashawishi ndugu zangu waislamu.[1] اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Kuna visa vingi kama hivyo.

[1] Kutoa maelezo ya kibinafsi ili kuwashawishi wafuasi na waumini ni desturi ya kale ya mawalii wetu lakini si sawa kwa mlinganizi wakawaida kufanya hivyo.

Hakika Mlinganizi aliyehitimu wa Dawat-e-islami ni yule ambaye ni hodari wa juhudi za kibinafsi.

Kumfanyia Dereva Juhudi Za Kibinafsi

اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Walinganizi wa Dawat-e-Islami wanaendelea kufuata sunna ya kufanya juhudi za kibinafsi na kuwaletea watu muamko wa kumfuata Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Wakati mwengine wao huniandikia kuhusu baraka wanazopata kutokana na juhudi zao. Haya hapa ni maelezo ya mmoja wao: “Watu wengi huja kuhudhuria ijtimai inayofanyika siku ya Alhamisi kila wiki Markazi ya Madani ya Dawat-e-islami Faīzān-e-Madīnaẖ, Bāb-ul-Madīnaẖ Karachi, kwa mabasi ambayo huegeshwa sehemu maalum.

Nilipokuwa napitia sehemu hii, nilimuona dereva akivuta bangi huku akisikiliza nyimbo ndani ya basi iliyokuwa tupu. Nilimwendea na nikazungumza nae kwa upole. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ, alizima redio pamoja na sigara. Nikiwa na tabasamu, nilimpa kaseti ya bayana ya kusisimua iitwayo: “Usiku Wa Kwanza Kaburini” ambayo aliiwasha mara moja. Nilikaa naye kuisikiliza kwani kukaa na kusikiliza kaseti pamoja na mtu ni njia moja ya kumshawishi. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ, alishawishika na bayana, akatubia dhambi zake na akaja pamoja nami Faīzān-e-Madīnaẖ kuhudhuria ijtimai.”

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Ndugu waislamu! Mumeona jinsi gani juhudi za kibinafsi zilivyo na faida na matokeo bora? Jaribu kumfanyia juhudi za kibinafsi kila muislamu kuswali. Kila unapokuja kuhudhuria ijtimai ima kwa basi au treni, mualike dereva kuhudhuria ijtimai ikiwa anaudhuru mpe kaseti, DVD au CD kusikiliza. Baada ya kusikiliza, ichukue na umpe nyengine.

Na badili yake chukua kaseti/CDs/DVDs zake za nyimbo, zifute na umtilie bayana halafu umrudishie. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ kwa njia hii tutaziangamiza kaseti za dhambi. Mtu hafai kuchoka kufanya juhudi za kibinafsi na kuwashauri wengine. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika Sura Żariyat, Juzuu ya 27, aya ya 55:

وَ ذَكِّرْ فَاِنَّ الذِّكْرٰى تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۵۵﴾

Na endelea kuwakumbusha;
maana ukumbusho huwafaa wanaoamini.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Makatazo Mawili Kutoka Kwa Mtume Mtukufu ﷺ

Wale wanaojishughulisha kupamba nyumba na maduka yao bila ya dharura wasome au wasikilize hadithi mbili za Mtume صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa makini:

1. Amekataza Kujenga Nyumba Bila Dharura

Sayyidunā Khabbāb رَضِیَ اللّٰهُ تَعَالٰى عَنْهُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, “Muislamu hupewa

thawabu kwa kila matumzi ila kwa mchanga huu.” *(Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, uk. 246, juz. 2, Ḥadīš 5182)*

Akishereheshea hadithi hiyo, mfafanuzi maarufu wa Qur’an Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَنَّان amesema, “Muislamu akitumia pesa kwa kula, kunywa, kuvaa na kadhalika, kwa nia njema hupata thawabu kwa sababu ni mambo ya kumsaidia mtu katika ibada. Lakini hakuna thawabu kujenga nyumba bila dharura. Kwa hivyo kupenda kukarabati nyumba mara kwa mara bila dharura ni kupoteza wakati na pesa.

Kumbuka! Makatazo hayo ni kuhusu kujenga majumba ya duniani bila dharura. Lakini kujenga misikiti na madrasa kwa nia njema ni aina ya ibada kwa sababu ni njia ya (kupata) thawabu. Vile vile ni amali njema kujenga nyumba kadiri ya dharura ili apate kumuabudu Allah عَزَّوَجَلَّ katika mazingira ya utulivu na salama. Watu wengine wanatabia ya kukarabati nyumba zao mara kwa mara kwa mitindo mipya.” *(Mirqāt, uk. 19, juz. 7)*

2. Hakuna Kheri Kujenga Bila Dharura

Sayyidunā Anas رَضِیَ اللّٰہُ تَعَالٰی عَنْہُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, “Matumzi yote ni kwa njia ya Allah عَزَّوَجَلَّ ila ujengaji wa majumba kwa sababu hauna kheri yoyote.” *(Sunan-ut-Tirmiżī, uk. 218, juz. 4, Ḥadīš 2490)*

Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْمَنَّان amesema, “Kujenga majumba ya kidunia bila dharura ni israfu-uharibifu wa pesa.” *(Mirqāt, uk. 20, juz. 7)*

Onyo Kutoka Kwa Bwana Wa Mawalii

Bwana wa Mawalii kipenzi wa Mwenyezimungu, Sheikh Abū Muhammad ‘Abdul Qādir Jīlānī قُدِّسَ سِرُّهُ النُّوْرَانِي siku moja alipitia nyumba ambayo bado ilikuwa ikijengwa. Akasema maneno yafuatayo:

أَتَبْنِيَ بِنَاءَ الْخَالِدِيْنَ وَ اِنَّمَا مَقَامُكَ فِيْهَا لَوْ عَقَلْتَ قَلِيْلٌ

لَقَدْ كَانَ فِيْ ظِلِّ الْاَرَاكِ كِفَايَةً لِّمَنْ كَانَ يَوْمًا يَّقْتَفِيْهِ رَحِيْلٌ

Tafsiri: Unajenga jengo la watakaoishi milele? Ilihali kukaa kwako ndani yake lau ungefahamu ni muda mfupi. Hakika kinamtosheleza kivuli cha mti msafiri ambaye humlazimu kupumzika siku moja na kuondoka siku ya pili. *(Tanbīĥ-ul-Mughtarīn, uk. 110)*

Walii wa Mwenyezimungu Alipomuona Mtu Akijenga Nyumba...

Sayyidī ‘Alī Khawāṣ عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الرَّزَّاق kila alipomuona Muongofu akijenga nyumba, alimlaumu na kusema, “Kila unachokitumia kujenga nyumba hii hutapata utulivu kwayo.” *(Tanbīĥ-ul-Mughtarīn, uk. 111)*

Kisa Chenye Mazingatio

Kijana kutoka Multan alichuma pesa nyingi kutoka nchi ya kigeni. Aliwatumia jamaa zake ili wamjengee nyumba nzuri ya

kupendeza. Kijana alituma pesa kwa miaka mingi. Hatimaye nyumba ilikamilika. Kijana aliporegea, matayarisho ya nyumba yalikuwa yamefikia kileleni; lakini lo! Kijana alikufa wiki moja kabla ya kuhamia nyumba yake. Alipelekwa kaburini badala ya nyumba yake ya kifahari."

Chumo La Miaka 100 Lisilo Na Uhakika Mbeleni

Mara nyingine mtu huwa hajali ila tu hajui yatakayompata. Imeelezwa katika *Ghunya-tuṭ-Ṭālibīn*, "Sanda za watu wengi zimeoshwa na ziko tayari lakini watakaozivaa hawajui. Wao wanazurura masokoni. Wengine makaburi yao yameshachimbwa tayari lakini wamepotea katika starehe. Wengine wanacheka lakini wakati wao wamaangamizo umekaribu. Ujenzi wa nyumba nyingi umekamilika lakini wakati wa kifo cha wenyewe pia umekaribia." *(Ghunya-tuṭ-Tālibīn, uk. 251, juz. 1)*

Ndugu wapenzi waislamu! Tunaishi maisha yakutojali duniani mpaka lini? Kumbuka! Mtu lazima ataondoka humu duniani kwa ghafla. Hayatakufaa mashamba mazuri, nyumba za kupendeza, makasri ya ghorofa, mali, almasi, lulu, dhahabu, fedha, umashuhuri wala mapato ya duniani. Mwili utainuliwa kutoka kwenye godoro laini na kuwekwa juu ya tandiko la mchanga kaburini bila mto.

Ni Mahali Pa Mazingatio

Ndugu waislamu! Ili kukumbuka kifo sikilizeni visa viwili vilivyochapishwa katika gazeti. Kumbuka kifo ni funzo kwa waliohai.

1. Kulingana na gazeti, msichana wa miaka 16 anayeishi Lahore amefariki papo hapo baada ya kitambara chake kuchomeka alipokuwa akichemsha maziwa.

2. Jiko la gesi lililipuka na kumuua mwanamke aliyekuwa akipika.

3. Watu wawili waliokuwa wamepanda juu ya garimoshi ili kumtazama kiongozi wa chama cha kisiasa katika msafara; walikufa baada ya vichwa vyao kugongwa na daraja ya garimoshi.

4. Aliingia ndani ya lifti lakini haikuwepo! Ndugu muislamu ameeleza, "Mwanamke mmoja Karachi, alikuwa akizungumza na mwenzake walipokuwa wakingojea lifti katika ghorofa ya nne. Mara mlango wa lifti ukafunguka; bila kuangalia, akaingia. Kumbe lifti ilikuwa bado haijafika. Akaporomoka kutoka ghorofa ya nne hadi ya chini na kufariki."

Yako Wapi Majumba Yakupendeza?

Ndugu waislamu! Yasikitisha watu wengi kuwa wanaipenda dunia lakini mapenzi ya ahera hawana. Kila mmoja anahamu ya mali ya duniani, viwanja na shahada za masomo. Ni wachache tu ambao wanajishughulisha na amali njema, msamaha, utajiri wa mapenzi ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na kupata Jannat-ul-Firdaus ambayo ni neema kubwa kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ. Enyi munaotafuta majumba ya duniani ya kifahari na makasri ya

kupendeza! Sikilizeni yasemwayo na Qur'an tukufu. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika, Sūraĥ Ad-Dukhān, juzuu ya 25, aya ya 25 -29:

كَمْ تَرَكُوْا مِنْ جَنّٰتٍ وَّ عُيُوْنٍ ﴿۲۵﴾ وَّ زُرُوْعٍ وَّ مَقَامٍ كَرِيْمٍ ﴿۲۶﴾ وَّ نَعْمَةٍ كَانُوْا
فِيْهَا فٰكِهِيْنَ ﴿۲۷﴾ كَذٰلِكَ ۫ وَ اَوْرَثْنٰهَا قَوْمًا اٰخَرِيْنَ ﴿۲۸﴾ فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ
السَّمَآءُ وَ الْاَرْضُ وَ مَا كَانُوْا مُنْظَرِيْنَ ﴿۲۹﴾

Mabustani mangapi na chemichemi ngapi waliziacha. Na mimea na mahali pazuri. Na neema walizokuwa wakijistareheshea. Namna hivi (tumewafanya). Na tukawarithisha haya watu wengine. Mbingu na ardhi hazikuwalilia wala hawakupewa muda.

Katika juzuu ya 22, aya ya 5 ya Sura Faṭir, Allah عَزَّوَجَلَّ amesema:

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ
فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۪ وَ لَا يَغُرَّنَّكُمْ بِاللّٰهِ الْغَرُوْرُ ﴿۵﴾

Enyi watu! Bila shaka ahadi ya Allah عَزَّوَجَلَّ ni ya haki. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala Yule mdanganyaji mkubwa (Iblisi) asikudanganyeni juu ya Allah عَزَّوَجَلَّ.

Tafakari Juu Ya Maisha Ya Ahera

Ndugu waislamu wapenzi! Fikirini! Kwa nini tumeletwa duniani? Lengo letu la maisha ni lipi? Tumeutumia vipi uhai wetu mpaka

hapa tulipofika? Kutafanyika nini wakati wa mauti, kaburini, Siku ya Hukumu, katika mizani, na katika daraja ya Ṣiraṭi? Kutakuwa kunafanyika nini katika makaburi ya jamaa na marafiki zetu waliokufa kabla yetu?

Tukitafakari kwa njia hii, tutapata kujitenga na anasa za dunia na tutahamasika kufanya amali njema kwa ajili ya kukumbuka kifo na vile vile tutapata thawabu, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ.

Ni Bora Kuliko Miaka Sitini Ya Ibada

Mtume Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم amesema, "Kutafakari (kuhusu ahera) kwa muda ni bora kuliko miaka sitini ya ibada" *(Al-Jāmi'-uṣ-Ṣaghīr, uk. 365, Ḥadīš 5897)*

Maiti Ya Siku 70

اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ, Kwa baraka ya mazingira ya Dawat-e-Islami, shirika lisilokuwa la kisiasa liloenea duniani kote la kulingania watu kufuata Qur'an na Sunna; mamilioni ya watu wanaozama katika bahari ya dhambi huokolewa. Hili ni shirika maalum la Madani la watu wa haki.

Ngojeni niwaeleze kisa cha kutia imani cha baraka za mazimgira ya Madanī ya Dawat-e-Islami: "Kulikuwa na mtetemeko mkubwa wa ardhi upande wa mashariki mwa Pakistani siku ya Jumamosi, Ramadhani tarehe 3, 1426 A.H. (Oktoba 8, 2005). Mamia ya watu waliangamia, miongoni mwao alikuwa msichana shahidi wa miaka 19 kwa jina Nasrin ʻAṭṭāriyyaĥ Bint-e-Ghulām Mursalīn

kutoka Mīrātasauliyān, Muzaffarabad (Kashmīr). Alikuwa akihudhuria Ijtimai za kila wiki za sunna za Dawat-e-Islami. Kwa sababu zisizoweza kuepukika, babake na jamaa zake iliwabidi walifungue kaburi lake saa nne za usiku siku ya Jumatatu; tarehe 8 Żul-Qa'da-tul-Ḥarām, 1426 A.H. (Desemba 10, 2005). Kaburi lilipokuwa likifunguliwa, waliokuwepo walisikia harufu nzuri ikitoka kaburini. Sanda ya Nasrīn 'Aṭṭāriyyaĥ ilikuwa vile vile kama ilivyokuwa siku ile alipozikwa. Mwili wake ulikuwa bado mzima hata baada ya siku 70 ya kifo chake cha kishahidi.

Allah عَزَّوَجَلَّ, amrehemu na atusamehe bila hesabu kwa baraka yake!

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Ndugu wote waislamu wanashauriwa kujaza kijitabu cha Madanī In'āmāt kufanya Fikr-e-Madīnaĥ, na wamkabidhi zimmadār wa eneo lao ifikapo tarehe 10 ya kila mwezi. Zaidi ya hayo, kusafiri kwa siku 3 na Madanī Qāfilaĥ kila mwezi pamoja na kuwashawishi ndugu waislamu wengine kwa kuwafanyia juhudi za kibinafsi kusafiri pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ mutaona baraka zake.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّد

Marejeleo

Al-Jāmi'-uṣ-Ṣaghīr, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Al-Mustadrak, Dār-ul-Ma'rifaĥ, Beirut.

Ashi'a-tul-Lam'āt, Quetta

Ghunya-tuṭ-Ṭālibīn, Dār Iḥyā-ut-Turāš-ul-'Arabī, Beirut.

Mirāt-ul-Manājīḥ, Zia-ul-Quran

Mishkāt-ul-Maṣābīḥ, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Mukāshafa-tul-Qulūb, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Musnad Abī Ya'lā, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Rauḍ-ur-Riyāḥīn, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Ṣaḥīḥ Bukhārī, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Ṣaḥīḥ Muslim, Dār Ibn Ḥazm, Beirut.

Shu'ab-ul-Īmān, Dār-ul-Kutub 'Ilmiyyaĥ, Beirut.

Sunan-ut-Tirmiżī, Dār-ul-Fikr, Beirut.

Tanbīĥ-ul-Mughtarīn, Al-Maṭbū'a-tul-Maīmniyaĥ.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Baraka Za Sunnah

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na siasa) sunna za Bwana Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah عزوجل pamoja na niya zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo ان شاء اللہ عزوجل tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume صلی اللہ تعالیٰ علیہ واٰلہٖ وسلم na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" ان شاء اللہ عزوجل

Kwa ajili ya kusuluhisha nafsi yangu nita fuata Madani In'amaat na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafilah. ان شاء اللہ عزوجل

MAKTABATUL MADINAH
Global Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan
Ph: +92-21-34921389 to 93, Ext: 1262
E-mail: translation@dawateislami.net Web: www.dawateislami.net